LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

LHRC

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

KIJARIDA KUHUSU

# HAKI ZA WATU WENYE ULEMAVU

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*




## Unaweza kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki kupitia

# #HakiKiganjani

SMS **0699695486**

Pakua AnroidApp ya **Haki Kiganjani**

hakikiganjani.humanrights.or.tz

***Usipotezee, toa taarifa sasa!***

KIJARIDA KUHUSU

# HAKI ZA WATU WENYE ULEMAVU

**Kimeandaliwa na:**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

# YALIYOMO


**1. UTANGULIZI ........................................................ 9**

**2. ULEMAVU ........................................................ 10**

**3. HAKI ZA WATU WENYE ULEMAVU NA WAJIBU WA JUMLA.... 12**

**3.1.Haki za Watu Wenye Ulemavu ........................................ 12**

3.1.1. Usawa na Kutokubaguliwa ........................................ 12

3.1.2. Kuishi kwa uhuru na kujumuishwa kwenye jamii ............ 13

3.1.3. Afya ........................................................ 13

3.1.4. Elimu ........................................................ 14

3.1.5. Kazi na Ajira ........................................................ 15

3.1.6. Ufikikaji na Upatikanaji ........................................ 16

3.1.7. Matembezi huru ........................................................ 17

3.1.8. Ushiriki katika maswala ya kisiasa na kijamii ...................... 17

3.1.9. Ushiriki katika maswala ya kiutamaduni, burudani, mapumziko na michezo ........................................ 18

**3.2.Kuishi na Hifadhi ya Jamii ........................................ 19**

**3.3.Wajibu wa Jumla ........................................................ 19**

3.3.1. Serikali/Nchi ........................................................ 19

3.3.2. Jamii/Familia ........................................................ 21

**4. HITIMISHO ........................................................ 22**

## SHUKRANI

Tunatoa shukrani kwa wanasheria walioshiriki kukirejea kijitabu hiki ili kuandaa toleo hili la nne hususani; Wakili Rose Nyatega, Wakili Joanitha Mutayob na Bi. Irene Nambuo pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

## DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma ya kusaidia jamii ya Watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama wangejua sheria. Ndiyo maana Kituo

kimeamua kutoa chapisho hili na mengine, kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi wa kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika kijitabu hiki tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia.

Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali umsaidie na mwenzako kupata usaidizi huu.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

# UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania mnamo mwezi Septemba, mwaka 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo ni Dar es Salaam na Arusha kuna ofisi ndogo.

# MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

# TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

# LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa unakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa kisheria.

# 1. UTANGULIZI

Kama makundi mengine, haki za watu wenye ulemavu zinatumia katiba kama msingi wake mkubwa. Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inazungumzia haki ya usawa.

Masuala ya watu wenye ulemavu yameendelea kuwa katika mipango ya kisheria kimataifa na hata kitaifa pamoja na harakati zake. Matukio muhimu kimataifa ni pamoja na; Azimio la Haki za Walemavu 1975, Mwaka wa kimataifa wa walemavu katika 1981, na programu za utekelezaji wa dunia kuhusu watu wenye ulemavu, 1982. Pia Tamko la Haki za binadamu la mwaka 1948 limetambua binadamu wote wanazaliwa sawa na huru bila kujali makundi. Mkataba wa Kimataifa wa kulinda haki na hadhi za watu wenye ulemavu nao umeendelea kutambua moja kwa moja watu wenye ulemavu kwa kuelezea haki na ulinzi wa watu hawa.

Ni dhahiri kwamba mfumo wa sheria kuhusu haki na ulinzi wa watu wenye ulemavu umechelewa sana Tanzania. Mwaka 2010, takribani miaka 50 tangu Tanzania ipate uhuru ndipo sheria namba 9 inayohusu haki za walemavu ilitungwa.

Watu wenye ulemavu wameendelea kunyanyaswa na kunyimwa haki zao katika nyanja mbalimbali za maisha na hii inapelekea wengi wao kuendelea kuishi kwenye umaskini. Kwa upande mmoja, ni muhimu watu wenye ulemavu kutambua haki na wajibu wao katika jamii.

## 2. ULEMAVU

Ulemavu kama ilivyotafsiriwa kwenye Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu; ni hali inayotokana na dosari mwilini au/na akilini ambayo inasababisha mtu kushindwa kutenda mambo ambayo kwa kawaida angetegemewa kuyaweza na hivyo kumletea mtu huyo kizuizi katika utekelezaji wa majukumu yake katika jamii.

Ulemavu kwa upana huainisha meneo matatu;

- Hali ya tatizo kadri linavyoonekana (impairment),
- Upungufu wa uwezo wa kutenda/kufanya jambo kwa njia ya kwaida kulinganana hali yake (disability),
- Kizuizi katika kutenda jambo (handicap) kutokana na hali ya ulemavu (disability)

Mtu mwenye ulemavu ni mtu ambaye mategemeo yake ya kupata, kumudu na kujiendeleza katika kazi yamepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na ulemavu unaotambulika mwilini, akilini na/au mfumo wa mitazamo wa jamii dhidi ya mtu huyo.

## KANUNI ZA MSINGI

Sheria ya watu wenye ulemavu namba 9 ya mwaka 2010 imejikita kwenye kanuni muhimu ambazo ni;

- Utu, uhuru wa kuchagua na kujitegemea;
- Kutokubaguliwa;
- Kushiriki na kushirikishwa kikamilifu katika Nyanja zote za maisha;
- Usawa wa fursa kwa watu wenye ulemavu;
- Ufikiaji na upatikanaji;
- Usawa wa wanawake na wanaume kwa watu wenye ulemavu;
- Kupatiwa huduma za msingi na mahitaji yao

# 3. HAKI ZA WATU WENYE ULEMAVU NA WAJIBU WA JUMLA

## 3.1. Haki za Watu Wenye Ulemavu

Sheria namba 9 ya mwaka 2010 inayohusu watu wenye ulemavu imeainisha haki za watu wenye ulemavu katika maeneo yafuatayo:-

### 3.1.1. Usawa na Kutokubaguliwa

i. Mtu mwenye ulemavu ni sawa kama mtu mwingine yoyote katika jamii na ana haki ya kutobaguliwa kwa namna yoyote kwa sababu ya hali ya kuwa na ulemavu;

ii. Mtu mwenye ulemavu ana haki ya kupata ulinzi sawa chini ya sheria dhidi ya matendo yote ya kibaguzi yatakayofanywa kwake.

**Angalizo**

Ikumbukwe kwamba kuchukua hatua chanya kwa nia ya kukuza usawa na kuondoa ubaguzi katika maeneo mbalimbali kwa kutofautisha, kutenga, kuajiri au kutoa kipaumbele kwa watu wenye ulemavu kwa sababu ya uwezo wao, haitafafsiriwa kama ubaguzi

### 3.1.2. Kuishi kwa uhuru na kujumuishwa kwenye jamii

Katika eneo hili, mtu mwenye ulemavu ana haki zifuatazo:-

i. Kusaidiwa na mamlaka husika kuishi kwa uhuru na kujumuishwa katika jamii zao;

ii. Mtu mwenye ulemavu hatoshurutishwa kuishi kwenye eneo maalum asilolitaka au kuchaguliwa jinsi ya kuishi ndani ya jamii;

iii. Huduma zilizopo ndani ya jamii zitarekebishwa ili kukidhi mahitaji binafsi ya watu wenye ulemavu.

### 3.1.3. Afya

Watu wenye ulemavu wana haki sawa ya kupata huduma bora za afya bila ubaguzi kwa kigezo cha ulemavu;

i. Mtu mwenye ulemavu atapata huduma za kiafya za aina mbalimbali kadri ya uhitaji wake zenye kiwango na ubora sawa kama zile zitazotolewa kwa watu

wengine;

ii. Huduma hizi za kiafya zitapatikana ndani ya jamii;

iii. Elimu na mafunzo itatolewa kwa watumishi wa afya ili kuongeza uelewa wao juu ya jinsi ya kuwatunza na kuwahudumia kiafya watu wenye ulemavu na kutoa uangalizi wenye ubora ule ule kwa kundi hili.

### 3.1.4. Elimu

i. Watu wenye ulemavu wana haki ya kupata elimu na mafunzo katika mazingira jumuishi kama watu wengine;

ii. Watoto wenye ulemavu wana haki sawa ya kujiunga katika shule za umma na binafsi kasoro tu pale ambapo mahitaji maalum ya kimawasiliano yanahitajikana atahitaji msaada wa ziada ili kunufaika kielimu;

iii. Kutotengwa kielimu kutokana na ulemavu. Marekebisho ya huduma yatafanyika ili kuridhisha na kuhakikisha wananufaika na elimu kadri wawezavyo

na wanatimiziwa mahitaji binafsi.

3.1.5. Kazi na Ajira

Watu wenye ulemavu wana haki ya kufanya kazi na kupata riziki kutoka kwenye kazi wanazojiamulia kufanya sawa na watu wengine. Sheria imetambua waajiri katika sekta za binafsi na zile za umma kuajiri watu wenye ulemavu. Mwajiri atatatakiwa;

i. Kuruhusu watu wenye ulemavu kujiunga pamoja na kuingia kwenye vyama vya wafanyakazi sawa na watu wengine kama yalivyomatakwa ya sheria;

ii. Kuondoa ubaguzi kwa vigezo vya ulemavu kuanzia hatua za kutafuta kazi, kuajiriwa na kuendelea na ajira, kuachishwa kazi, usawa wa malipo, usawa wa fursa na usalama kazini;

iii. Kuwezesha watu wenye ulemavu kumudu kazi kwa kutengeneza mazingira wezeshi na kuhakikisha marekebisho ya mara kwa mara yanafanyika kukidhi mahitaji yao;

Kutoa na kuendeleza mafunzo yakuwasaidia watu wenye ulemavu kazini na kudumu katika ajira zao.

Muhimu:

Kila mwajiri mwenye wafanyakazi kuanzia ishirini (20) na kuendelea anawajibu wa kuhakikisha kwamba asilimi tatu (3%) ya wafanyakazi wake ni watu wenye ulemavu.

Ni kosa kisheria kutokuajiri mtu mwenye ulemavu mwenye kigezo cha kazi husika bila kuwa na sababu ya msingi.

### 3.1.6. Ufikikaji na Upatikanaji

Sheria inatoa haki ya watu wenye ulemavu kufikia na kupata huduma zote za jamii na kupata msaada stahiki kama vile wasomaji, wakalimani, lugha za alama na wasindikizaji. Sheria inaondoa vizuizi vinavyowapata watu wenye ulemavu katika hali ya kuishi na kujitegemea kama wanavyotaka. Vizuizi vinakatazwa;

i. Kwenye miundombinu hususani majengo ili kuwezesha ufikikaji kirahisi kwa watu wenye ulemavu;

ii. Kwenye huduma zote na maeneo ya umma na kwamba zitaweka viwango

vya ufikikaji kwa watu wenye ulemavu;

iii. Kwenye upatikanaji habari na mawasiliano pia katika huduma za kielektroniki.

### 3.1.7. Matembezi huru

Watu wenye ulemavu wana haki ya kutembea katika hali na muda wanaopenda. Watasaidiwa kupata nyenzo na mazingira wezeshi ya kumudu kutembea wao wenyewe na wanaojishighulisha nao. Wale wanaojihusisha na kutengeneza nyenzo hizi watahakikisha kwamba nyenzo hizo zinafaa kumudu watu wenye ulemavu na kufanya mabadiliko kadri itakavyohitajika.

### 3.1.8. Ushiriki katika maswala ya kisiasa na kijamii

Watu wenye ulemavu wanauwezo wa kushiriki kikamilifu katika maswala ya kiasiasa na kijamii kama watu wengine bila ubaguzi. Kisiasa; haki ya kupiga kura katika mchakato ambao ni rahisi na unafikika. Haki ya kuchaguliwa na kushika madaraka, kujishirikisha na asasi za kiraia na vyama vya

vyenye mtazamo wa kisiasa. Watu wenye ulemavu wana haki sawa ya kujihusisha na mambo ya kiserikali na ya umma.

### 3.1.9. Ushiriki katika maswala ya kiutamaduni, burudani, mapumziko na michezo

Watu wenye ulemavu wana haki sawa ya kushiriki kwenye burudani, mapumziko, michezo na maswala ya kiutamaduni kama watu wengine kwa kupata;

i. Pragramu za televisheni, filamu, maonyesho ya kitamaduni;
ii. Machapisho katika muundo wanaoweza kuelewa;
iii. Kuyafikia maeneo ya kitamaduni kama Makumbusho na nyumba za sinema bila vizuizi;
iv. Kutambuliwa rasmi kwa lugha na tamaduni zao;
v. Kushiriki katika michezo kwenye ngazi mbalimbali;
vi. Fursa za kuandaa, kushiriki na mafunzo kwenye shughuli za michezo;
vii. Huduma za kuwasaidia kushiriki

kikamilifu katika michezo.

### 3.2. Kuishi na Hifadhi ya Jamii

Watu wenye ulemavu wana haki ya kupata hifadhi ya jamii bila kubaguliwa kwa kigezo cha kuwa na ulemavu. Wanaweza kupata huduma, vifaa na misaada wanayohitaji. Hususani wanawake wanaweza kupata programu za kuwasaidia kuondokana na umaskini. Wanaweza pia kunufaika na misaada ya kifedha pamoja na programu za nyumba na makazi.

### 3.3. Wajibu wa Jumla

Kila mtu anawajibu wa kulinda na kutetea haki za watu wenye ulemavu. Wajibu pia unatofautiana kutokana na makundi mbalimbali kama ifuatavyo;

3.3.1. Serikali/Nchi

i. Kuhakikisha haki na utu wa watu wenye ulemavu unaheshimika;
ii. Kufuta au kurekebisha sheria na desturi zinazobagua watu wenye ulemavu;
iii. Kuonyesha kuwa watu wenye ulemavu wana haki sawa kama watu wengine;
iv. Kuendeleza programu na mafunzo

ya kufanya watu waendelee kuwa na ufahamu tosha juu ya haki za watu wenye ulemavu;

v. Kuwalinda kisheria watu wenye ulemavu;

vi. Kutungwa sheria, sera na kuchukua hatua zingine ili kuhakikisha watu wenye ulemavu wanalindwa;

vii. Uheshimikaji wa kutoa na kupokea habari sawa na wengine;

viii. Kuhakikisha upatikanaji wa vifaa na huduma kwa urahisi na gharama nafuu kwa watu wenye ulemavu;

ix. Kutoa fursa sawa za mafunzo ya ufundi stadi, elimu na ujifunzaji katika maisha sawa na watu wengine na kufanya marekebisho stahili kuwafanya watu wenye ulemavu kunufaika kikamilifu;

x. Kukusanya taarifa na takwimu juu ya watu wenye ulemavu ili kuweza kutumika kwenye mipango na utekelezaji wa programu kwa manufaa yao na pia kuweza kutoa hizi taarifa na kuhakikisha watu wenye ulemavu wanaweza kuzisoma na kuzielewa.

### 3.3.2. Jamii/Familia

i. Kutowatesa, kuwatendea au kuwaadhibu kikatili au kiudhalilishaji watu wenye ulemavu;

ii. Kuwaheshimu watu wenye ulemavu kimaumbile na kiakili kama watu wengine;

iii. Kuheshimu maisha yao ya kifamilia na familia zao;

iv. Kuwasaidia kushiriki na kujumuishwa katika shughuli mbalimbali kwenye jamii zao;

v. Kutokuwabagua watu wenye ulemavu;

vi. Kupigana dhidi ya Imani potofu na chuki kuhusu watu wenye ulemavu;

vii. Kutoa uangalizi na kuwatunza watu wenye ulemavu;

# 4. HITIMISHO

Katika kitini hiki, tumeweza kujifunza mambo mbalimbali kama vile haki za watu wenye ulemavu na wajibu wa serikali na jamii kwa watu wenye ulemavu kama zinavyoainishwa kwenye sheria ya watu wenye ulemavu namba 9 ya mawaka 2010.

Ndugu msomaji, ni matumaini yetu kuwa kitini hiki kimekupa ufahamu na mwanga kuhusu haki hizo; na ufahamu juu ya wajibu wa nchi kupitia serikali pamoja na jamii. Hii itakusaidia wewe binafsi na pia kuweza kuwasaidia wengine kuhusu kutambua na kutetea haki za watu wenye ulemavu.

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU**
S. L. P. 75254, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**DODOMA OFFICE**
Kitalu na 22. Area D,
S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**Ofisi ya Arusha**
Barabara ya Olerian, Olosiva Kitalu Na. 116/5,
Sakina kwa Idd, Arumeru
S. L. P. 15243, Arusha - Tanzania
**Simu:** +255 27 2544187
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**Kituo cha Msaada wa Sheria**
Mtaa wa Isere - Kinondoni
S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*